

Mwingilianomatini katika Utanzu wa Riwaya: Mshabaha kati ya *Nyuso za Mwanamke na Wenye Meno*

Kinyua Alex, Mwenda Mbatiah na Simon Ongarora

Chuo Kikuu cha Nairobi

Ikisiri

Kazi za kifasihi huhusiana, hurejeleana na huingiliana katika mchakato wa kuandikwa kwake, lakini mambo haya hujibainisha kwa uwazi zaidi katika mchakato wa upokezi na ufasiri wa kazi hizo. Bakhtini, mwasisi wa Nadharia ya Mwingilianomatini, anahoji kwamba utanzu wa riwaya una uwezo na wasifu wa kutumia na kushirikisha kiutunzi nduni za tanzu nyingine na bado utanzu huu ukabakia na sifa zake kama utanzu. Kwa mfano, riwaya inaweza kuhusisha na kushirikisha kiutunzi sifa au nduni ya mazungumzo ambayo aghalabu hubainika katika utanzu wa tamthilia au ikahusisha kanuni za ushairi na bado ikabakia kama riwaya. Mnadharia huyu anasema kwamba utanzu wa riwaya una upekee kwa sababu una uwezo wa kuchota sifa, mbinu na mikakati ya kiutunzi ya tanzu nyingine na kuzijumlisha katika kurutubisha muundo na usanifu wake kwa njia anuwai. Sifa hizi za kuhusiana, kurejeleana na kuingiliana kwa nduni za kiutunzi, ni uhalisia unaojitokeza kwa wingi katika tungo za Said Ahmed Mohamed. Kauli hii inahalisi kuhoji kuwa kuna kiasi kikubwa cha mwingilianomatini kinachojitokeza katika kazi za mtunzi huyu. Hali hii inashawishi na kuchochea shauku ya kiutafiti kutaka kubaini kama Said Ahmed anajikariri kiutunzi au kama kuakisika kwa nduni sawia kutoka kazi moja hadi nyingine ni ufundi wa kukuza na kuimarisha mbinu zake za kiutunzi. Hivyo, mchango wa makala hii katika kuziba pengo hilo ni kuchunguza jinsi riwaya mbili za Said Ahmed: *Nyuso za Mwanamke* (2010) na *Wenye Meno* (2014) zinavyoingiliana katika vipengele vya maudhui na uhusika. Usampulishaji wa kimakusudi umetumika kuteua kazi hizi. Kwa ujumla, mwelekeo wa makala ni wa mwingilianomatini.

Maneno Muhimu: *Mwingilianomatini, Riwaya, Usemezano, Utunzi*

Utangulizi

Miongoni mwa watunzi wa riwaya ambao wameendelea kuacha taathira kubwa katika utanzu huu ni Said Ahmed Mohamed. Kama, Euphrase Kezilahabi, Said Ahmed ni mwandishi na msomi ambaye ametoa mchango katika kuipévusha riwaya ya Kiswahili. Ametangamana na fasihi za kilimwengu na kuathiriwa nazo. Athari hizo zinajitokeza wazi katika baadhi ya riwaya zake hasa za hivi karibuni ambazo zimeonyesha kuwapo kwa sifa za kinjozi au kifantasia. Kazi zinazodhihirisha sifa hizi ni zile ambazo ametunga katika awamu ya pili ya uandishi wake na ambazo tunahakiki katika makala hii. Katika awamu ya kwanza, kazi zake zilijikita katika masuala ya jamii yake ambapo aliihakiki na kubainisha migogoro yake. Zimejikita katika ufafanuzi wa hali kama inavyobainika katika dunia halisi na masuala ambayo yanaweza kudhihirika kihistoria. Riwaya zake za awamu ya kwanza ni: *Asali Chungu* (1977), *Utengano* (1980), *Dunia Mti Mkavu* (1980), *Kiza Katika Nuru* (1988) na *Tata za Asumini* (1990).

Katika kipindi cha pili, itikadi ya Said Ahmed inaonekana kubadilika alipohamia Ulaya. Alitagusana na fasihi za Kiulaya hasa kazi kama vile *The Tin Drum* na nyinginezo na pia kupata hadhira tofauti kule. Masuala ambayo anaandikia katika awamu ya pili ya utunzi wake yanavuka mipaka ya kitaifa na yanayohusu ulimwengu mzima. Masuala ambayo yanahusu ulimwengu halisi na ulimwengu wa kiajabu ambapo mpaka baina yake hauwekwi bayana. Riwaya za kipindi hiki zilizochapishwa kufikia kuandikwa kwa makala hii ni: *Babu Alipofufuka* (2001), *Dunia Yao* (2006), *Nyuso za Mwanamke* (2010), *Mhanga Nafsi Yangu* (2012) *Mkamandume* (2013), *Kamwe si Mbali Tena* (2014) na *Wenye Meno* (2018).

Wamitila (2008: 354), anasema kuwa Said Ahmed Mohamed anaweza kusemwa kuwa ni mtunzi ambaye ametunga kazi zinazowakilisha upekee wa kiutunzi unaobainisha ujitokezaji wa mwingilianomatini katika maendeleo yake ya kiutunzi. Anamweleza Said Ahmed kama mtunzi aliyehusisha mitindo ya kimajaribio na mwingilianomatini katika kazi zake za baadaye ambazo tunarejelea kama kazi za awamu ya pili katika makala hii.

Utafiti huu umeongozwa na Nadharia ya Mwingilianomatini. Allen (2000: 35) anafafanua kuwa, kazi za kifasihi huundwa kutokana na kazi zilizotangulia. Msomaji wa matini fulani hujiingiza katika mtandao wa mahusiano ya matini na hivyo, maana itakayopatikana huwa ni kilichoko baina ya matini husika na nyingine yoyote ile inayohusiana nayo. Hali hii ndiyo Allen anairejelea kama mwingilianomatini. Anaendelea kusema kuwa, kazi yoyote ya sanaa haiwezi kuangaliwa kwa upekee wake kwa vile kazi hii iliundwa kutokana na kazi nyingine ya awali iliyohusiana nayo.

Bakhtin alijishughulisha na jinsi semi au matini hupata maana yake kutokana na kazi zilizoitangulia. Bakhtin (1981), anasema kuwa semi zote huwa ni jibu la semi na ruwaza za maana za awali. Kwa mujibu wa kauli hii, hakuna matini iliyoandikwa iliyo na upekee wa maana kwa vile matini inayochunguzwa huhusishwa na nyingine za awali. Aidha, mnadharia huyu alizungumzia dhana ya usemezano. Anafafanua kuwa semi zote huwa ni za kiusemezano na maana ya semi hizi hutegemea semi za awali na namna zinavyopokelewa na hadhira lengwa. Kulingana na Bakhtin, semi zinazotolewa huwa na athari za semi za awali. Hali hii ndiyo Kristeva alikuja kuirejelea kama mwingilianomatini.

Mawazo ya Kristeva yamewekewa msingi na yale ya Bakhtin. Dhana inayomwathiri Kristeva katika uhakiki wa Bakhtin ni ile ya usemezano ambapo katika matini moja kunapatikana wingi wa sauti. Hivi ni kumaanisha matini za kifasihi hurejeleana kwa namna moja au nyingine kiasi kwamba zinachangizana katika kuzalisha maana. Baadhi ya mihimili mikuu ya Nadharia ya Mwingilianomatini ni pamoja na:

- i. Hakuna matini inayoweza kujisimamia kivyake. Matini hupata maana kwa kuhusishwa na matini nyingine za awali.
- ii. Matini za kifasihi huchota, huiga, hubeza na hurejelea matini za awali.
- iii. Matini za kifasihi hujengeka katika mifumo ya kanuni na tamaduni zilizowekwa na matini za awali. Mwandishi anapoandika matini yake husoma matini za awali.
- iv. Matini yoyote ile, huwa ni mabadiliko ya mpangilio wa matini tangulizi. Kauli inayonukuliwa huelezwa upya kwa kuambathishwa katika muktadha mwingine wa kiisimu na kijamii.
- v. Maana ya maneno ya mwandishi haitokani na upekee wake bali hutokana na mifumo ya lugha na utamaduni wake. Mwandishi huwa na jukumu la kukusanya na kupanga yaliyomo katika mfumo wa lugha. Matini itakayoundwa itapata maana kutokana na mfumolugha ilimoundiwa.

Muhtasari wa Riwaya ya *Nyuso za Mwanamke*

Katika riwaya ya *Nyuso za Mwanamke*, msichana Nana anajipata katika jamii iliyotawaliwa na mfumo wa ubabedume. Bwana Hila, ambaye ni baba yake Nana, ni kiongozi fisadi na katili ambaye anaendelea dhuluma dhidi ya tabaka la chini. Aidha, Bwana Hila anamchukulia mwanamke kama chombo cha kujistarehesha na kuyumbishwa kama tiara. Anamwona mwanamke kama kiumbe wa kusalia nyumbani na kungoja kumstarehesha mwanamume. Kwa upande wake, Nana ni mwanamke shupavu na mwenye msimamo thabiti. Anapinga juhudi za baba yake za kumtafutia mume. Anataka awe na uhuru wa kujieleza na kujiamulia. Anakataa tajiri aliyetafutwa na baba yake na kumpenda maskini ambaye ni mpiga-gita. (Uk. 47). Anapochoshwa na dhuluma chini ya mfumo wa kuumeni, Nana anafunga safari ya kuzaliwa upya; safari ya kujisaka na kujifahamu. Anataka kuzaliwa upya ili auasi mfumo wa ubabedume ambao unaendelea unyanyasaji dhidi ya jinsia ya kike. Katika safari yake, Nana anadhihirisha kuwa mwanamke si dhana nyepesi. Ana nyuso nyingi ambazo ni tata na ngumu kuzieleza na kuzielewa.

Muhtasari wa Riwaya ya *Wenye Meno*

Wenye Meno ndilo chapisho la karibuni zaidi miongoni mwa riwaya za Said Ahmed. Wahusika wakuu katika riwaya hii ni mwanamke jasiri kwa jina Halima na Mwenye Meno. Mwenye Meno anawakilisha tabaka la juu lenye mamlaka, utajiri na vyombo vya dola. Tabaka hili lina hamu isiyo na mwisho. Linaiendesha jamii jinsi linavyotaka na kila kitu kipo chini ya mamlaka yao: mashamba, magari, wanawake, burudani n.k. Halima kwa upande wake, ni mwanamke shupavu, msomi na mwanamapinduzi. Anashiriki katika utafiti wa kuwachunguza watu wakubwa waliogeuka funza wa kulinyonya tabaka la chini. Anachapisha matokeo ya utafiti wake katika gazeti la *Habari Motomoto*. (Uk. 20). Halima vilevile, anawasilishwa kama mwanamke anayefaulu kuidengua kasumba inayoendesha mfumo wa kuumeni kuwa mwanamume ana uwezo kuliko mwanamke. Anapinga vikali jaribio la Mwenye Meno la kumnunua kwa pesa. Analiona tendo hilo kama ishara ya kumvunjia mwanamke heshima. Hatimaye, Mwenye Meno anaungama kuwa Halima ni shujaa mwenye uhuru wake wa kusema anachotaka bila kuogopa, uhuru usioendesha na tamaa ya pesa na uhuru wa heshima ya uke. (Uk. 207).

Mwingilianomatini wa Kimaudhui katika *Nyuso za Mwanamke na Wenye Meno*

Kimani na Chimera (1999: 21) wanasema kuwa maudhui ni ujumbe wa jumla kuhusu matukio, kitu, wahusika au hali ya maisha kama inavyojitokeza katika kazi ya kifasihi. Naye Wamitila (2008: 521), anasema kuwa maudhui ni jumla ya masuala au mambo yanayoshughulikiwa katika kazi ya kifasihi. Masuala haya hutokana na jinsi mtunzi au mwandishi anavyoikuza mada ambayo ni msingi wa utunzi wa kazi yake. Sehemu inayofuata inajadili jinsi riwaya zilizoteuliwa zinavyohusiana na kurejeleana katika kipengele cha maudhui.

Mwingilianomatini katika Maudhui ya Ubabedume

Katika riwaya mbili tunazohakiki, jinsia ya kike inadhalihiwa na ile ya kiume. Haya ndiyo maswala yanayoangaziwa na wahakiki Mary Egleton na Ross Murfin (1991), wanapoeleza jinsi mwanamke wa Kiafrika alivyonyimwa uhuru wa kujiamulia mume wake, uhuru wa kujieleza na mila na desturi zinazomkandamiza. Bwana Hila katika *Nyuso za Mwanamke*, ni mhusika mwenye taasubi ya kiume. Anamzaba kofi Nana ambaye ni binti yake na kumlinganisha na marehemu mkewe. Aidha, Bwana Hila anashikilia kuwa sharti amtafutie binti yake mume. Anakusudia kumwoza bintiye katika familia ya kitajiri japo Nana anapinga na kusababisha mgogoro unaompelekea kuzabwa kofi.

Nana anasimulia jinsi wanaume wanavyowatazama wanawake kama watu wasiokua. Wanaokua ni wao tu wanaume. Hili linaelezwa katika dondoo ifuatayo:

Akina baba bado wanadhani wanaweza kuvidhibiti vizazi vipya vilivyopo na vinavyokuja. Kwao, dunia haibadiliki kamwe. Giza limezingira kila pahala lakini bado wanadhani mamlaka yao yanang'ara urenda wa nguvu. Wanachukulia tu kuwa watoto wao hawakui. Watu wote kwa hakika hawakui wanavyohisi wao. Watoto, vijana na hasa wanawake hawakui. Wanaokua ni wao tu. (Said Ahmed, 82).

Mwanamke katika jamii ya Nana anachukuliwa kama bidhaa za kuuzwa hata bila ya hiari yake. Mama yake Nana aliozwa kwa lazima. Tunaelezwa kuwa hii ilikuwa mojawapo ya ndoa za kulazimishwa. Kulingana na Nana, kila mwanamke katika jamii yake alikuwa na uso wake ulioashiria dhuluma za aina mbalimbali. Tazama:

Kila mwanamke alikuwa na uso wake. Nyuso za vitoto na vigori zinazoonyesha halaki mapema kabla hata ujanajike haujafumbuka na kunawiri ndani ya nafsi zao. Nyuso za wanawari zinazosawijika baada ya kubijwa na kukabwa na kubakwa. Au zinazotazamiwa kuozwa wanaume mapema au wanaume wasiowataka wala kuwachagua. Nyuso za walioolewa zinazosunyaa kwa joto kali la ndoa kabla hata ndoa yenyewe haijasimama vizuri. Nyuso za wanawake wanaonyang'anywa mirathi yao, kwa sababu tu

wamezaliwa wanawake. Wengi wa hawa walikufa huku wa hai. Walikufa kabla siku si zao. Nyuso na nyuso na alkuki ya nyuso za wanawake... (Said Ahmed, 183).

Katika kipindi cha *Dukuduku* kwenye *Televisheni Yetu* kilichoanzishwa na Nana, wanawake wanajadili dhuluma wanazopitia mikononi mwa wanaume. Mhusika Shemsa anaeleza jinsi jamii yake ilivyotawaliwa na mfumo wa kuumeni. Anasema kuwa katika jamii yake haikuwa kawaida kwa binti kumchagua mume aliyependa. Mwanamke mwingine kwa jina Bi. Kivumbasi, anatoa mchango wake wa namna sauti ya mwanamke ilivyokuwa imezimwa katika jamii yake. Haikuwezekana kwa mwanamke kukataa posa kwa vile hilo lilikuwa jambo kubwa. Ilipotokea, wazee walitumia kila hila na ilipobidi walitumia nguvu na maapizo yaliyoambatana na kukosa radhi za wazazi wake na Mungu. (Uk. 210).

Kauli ya mwanamume mmoja aliyechangia mjadala ule inadokeza jinsi ubabedume ulivyokita mizizi katika jamii. Baada ya kupatiwa nafasi na Nana, mwanamume alitoa kauli ifuatayo:

Tokea zamani wazazi waliona bora waondoe bidhaa mbovu njiani. Yaani mtoto wa kike ni bidhaa mbovu itakayokuja kuwaozea ndani wazazi huku wanaona. Mtoto wa kike akishakuwa mwari, basi keshakuwa mzigo au bidhaa mbovu kwa familia. Ni mtego kwa heshima na familia nzima pia. (Said Ahmed, 210).

Bi. Mkubwa anahadithia juu ya unyanyasaji aliopitia chini ya wanaume. Alilazimishwa kuolewa na Bw. Hila ambaye aliamini kuwa mwanamke ni chombo cha kumstarehesha mwanamume. Alipewa kila alichotaka isipokuwa uhuru wa kutoka nje ya nyumba. Baada ya kuondoka kwenye ndoa hiyo, anaolewa na Simai ambaye anampiga kila kuchao. Anampiga kibao mpaka anavimba uso na kuvunjika mkono kwa kuchelewa kupika. Anapigwa mpaka anaamua kufunga virago na kuondoka. Maji yanazidi unga Bi. Mkubwa anapojiriwa na mwanamume mwenye asili ya Kihindi kwa jina Selemani Kijogoo. Kijogoo anamwona Bi. Mkubwa kama kifaa cha kukonga tamaa yake ya mapenzi. Anamshika kwa nguvu na kumbaka. Hatimaye, Bi. Mkubwa analazimika kuridhia utumwa wa kitandani na utumwa mwingine wa nje na ndani bila kulalamika. (Uk. 290).

Sawa na Bwana Hila katika *Nyuso za Mwanamke*, Mwenye Meno katika riwaya ya *Wenye Meno*, anaamini kuwa mwanamke ni chombo cha kumstarehesha mwanamume. Tunamwona akiwanunulia wanawake aliokuwa na hamu nao magari, mapambo ya dhahabu, nguo, vipodozi na manukato ya bei ghali. Palipotokea wanawake walioonekana kuwa wagumu, Mwenye Meno anawajengea hata majumba ya ghorofa mradi atimize uchu wake wa mapenzi.

Mbali na kwamba Shahida ni mpenziwe Mwenye Meno, Mwenye Meno anamgeuza mjumbe wa kumtafutia vipusa. Shahida analalamika kwa uchungu kuwa Mwenye Meno aliuchukua mwili wake akaupondaponda na kuuharibu. Falsafa inayomwongoza Mwenye Meno ni kuwa mwanamke ni tiara inayozungushwa kwa pesa. Hii ndiyo maana anawatazama wanawake wanaokaidi matakwa yake kama waliokosa hisani na fadhila. Kulingana naye, thamani ya mwanamke ni sawa na bidhaa za kifahari anazowanunulia hivyo inaakisi kubadilisha bidhaa na zingine. (Uk. 132).

Mwingilianomatini katika Maudhui ya Utabaka

Kulingana na Njogu, K na Wafula, R (2007), jamii hugawika katika makundi mbalimbali yasiyo na usawa. Aghalabu, makundi haya hutegemea uwezo wa kiuchumi, mielekeo ya kisiasa, dini na elimu. Uhalisia huu unajitokeza katika riwaya zinazohakikiwa. Katika kazi hizi, kuna tabaka la juu ambalo ni la matajiri wenye hela na mamlaka na kwa upande mwingine, kuna maskini wa tabaka la chini ambao wanadhulumiwa kimapenzi na kiutawala na tabaka la juu. Nana katika riwaya ya *Nyuso za Mwanamke*, anaeleza juu ya sherehe nyingi zilizofanyika nyumbani kwao. Waalikwa walikuwa watu wakubwa wenye hela na vyeo kama baba yake. Wachochole hawakukubaliwa katika sherehe hizo isipokuwa watumishi wa nyumbani wa Bwana Hila. Nana anakaulisha kwa kusema:

Kwa jumla, watu wote hao na zaidi ya hao, walikuwa wageni wetu siku ya sherehe – siku ya *party*. Kulikuwa hata na wale walioalikwa kutoka nje ya nchi kwenye zile zilizonuiwa kuwa *party* kubwa kuliko zote miongoni mwa *party* zetu. Mradi tu wawe watu wakubwa kama

sisi. Hakuna mchochole aliyealikwa kwenye sherehe hizo, isipokuwa watumishi wetu ambao walikuwa si watumishi mburumatari kama watumishi wa watu wengine wasiojipata kama sisi. (Said Ahmed, 31).

Pengo baina ya tabaka la juu na lile la chini linasisitizwa na Nana kupitia utajiri wa baba yake. Nana anaeleza kuwa baba yake alikuwa mkubwa na mambo yake yalikuwa makubwa. Anatuambia kuwa baba yake alimiliki vitu ambavyo havikupatikana na watu wengine. Kimsingi, hii ni jamii ambayo imegawika kitabaka hivi kwamba watu wachache wanamiliki utajiri mkubwa huku maskini walio wengi wakiangamia. (Uk. 29).

Jumba la kifahari la Bw. Hila linawaka taa kwa fujo wakati vitongoji vya hapo karibu vinazama katika giza. Hivi ndivyo mwandishi anagotanisha mandhari ya tabaka la juu na yale ya tabaka la chini kupitia mhusika Nana:

Jumba letu lilikuwa pandikizi la jumba, kama vile limeshushwa kwa miujiza au kwa mbinu na fahari za uchawini. Ingawa likimeremeta mataa ya rangi mbalimbali, kwangu mimi leo lilitisha. Rangi zilizojitupa juu ya jimwili lake zimetatizana. Baadhi zinakonyezana na nyingine zinakogeshana na jumba lenyewe likajiona limefaidika. Taa ziliwaka kwa fujo wakati kwenye vitongoji vya karibu na hapo kulikuwa na giza tupu. (Said Ahmed, 35).

Maudhui ya utabaka katika riwaya ya *Wenye Meno* yanazungumziana na yale ya riwaya ya awali ya *Nyuso za Mwanamke*. Sawa na Bw. Hila, Bw. Mwenye Meno anawakilisha tabaka la juu linaloogelea kwenye utajiri mkubwa. Nguli wa riwaya ya *Wenye Meno* anayejulikana kama Halima, anashangazwa na pesa za Mwenye Meno ambazo anatumia kiholela huku maskini wengi wakiangamia kwa janga la njaa. Halima anashangaa:

Lilipotokea swali la wanawake wagumu, mtunuki aliwajengea hata nyumba za ghorofa. Mtu akigeuza kichwa na kutafakari, ataona kwamba huo ni mchezo wa kitoto kwa mtunuki, kwani kwake ni jambo dogo tu! Mchezo wa kitoto ndiyo, lakini pesa zote hizo alizipata wapi? Ardhini au mbinguni? Ajabu kubwa ni kwamba nchi hii ina maskini wengi wanaokosa hata mlo mmoja kwa siku. Hivi vilikuwa vita vya wasakatonge na walatonge wanaopata pesa kwa urahisi! (Said Ahmed, 84)

Mandhari anakoishi Mwenye Meno yanashabihiana na yale ya Bwana Hila. Jumba la Bw. Hila linaelezwa kama pandikizi la jumba nayo makaazi ya Mwenye Meno yamesimama katika eneo lililokuwa nusu dunia. Tunaeleza:

Alipokuwa akikaribia mzunguko wa makaazi ya Mwenye Meno, Halima alishangaa jinsi upeo wa eneo la ardhi ya Mwenye Meno lilivyo. Alitupa macho pande zote za tambarare ili aone mwanzo na mwisho wa mipaka ya makaazi ya bwana huyo. Yule mzee wa rafiki yake Muuza Mdafu, na mfanyikazi wa Mwenye Meno, alimweleza Halima pahala hapo na ukubwa wa eneo la bosi wake kwa kutia chuku kuwa eneo hilo lilikuwa nusu ya dunia. (Said Ahmed, 153).

Taswira ya jinsi jamii ilivyogawika kitabaka inashadidiwa na Mwenye Meno mwenyewe anapoungama kuwa dunia imegawika katika makundi mawili kitabaka:

Kumbe kuna mpasuko duniani. Mpasuko wa wachache na wengi. Wachache ndio wenye nguvu ya pesa na mabilioni yasiyohesabika. Pia, nguvu za kutawala na kuamua. Kikundi ambacho kinaweza kufanya chochote katika dunia hii. Kisha kuna nguvu za silaha zinazoangamiza wale walio wengi. (Said Ahmed, 184).

Mwingilianomatini katika Maudhui ya Nafasi ya Mwanamke

Katika makala yao, 'The Role of Women in Today's Society,' Yadav D.S na Kumar K.J (2021), wanafafanua kuwa nafasi ya mwanamke katika jamii imeimarika tofauti na ilivyokuwa hapo awali ambapo mwanamke alilazimika kusalia nyuma ya kivuli cha mwanamume. Mwanamke sasa anajitambua, kujimudu na kujitegemea kwa njia mbalimbali hasa kiuchumi. Aidha, wataalam hawa wanashikilia kuwa mwanamke amepiga hatua katika nyanja mbalimbali zikiwamo siasa, elimu, michezo na nyinginezo. Katika bunilizi tunazochunguza, mwanamke amepatiwa kipaumbele katika shughuli za kijamii. Mwanamke amepatiwa nafasi ya kimsingi katika mchakato wa kuikomboa jamii yake. Mwandishi amemsawiri mwanamke kama mshiriki mkuu katika juhudi za kujikomboa na kuikomboa jamii yake. Wanawake wote wawili (Nana katika *Nyuso za Mwanamke* na Halima katika *Wenye Meno*), wanapinga tamaduni za jamii zao za mwanamke kutafutiwa mume wa kumwoa. Wanakaidi mielekeo ya jamii zao ya kumwangalia mwanamke kama bidhaa za kununuliwa kwa pesa.

Nana anakataa kuozwa kwa mwanamume tajiri aliyechaguliwa na baba yake. Anakataa zawadi ya gari la kifahari aina ya *Volvo* kutoka kwa kijana tajiri kwa jina Dusa. Anataka awe huru kujitafutia mume. Anayejichagulia ni mwanamume wa tabaka la chini asiye na pesa. Nana anaishia kumpenda mpiga-gita ambaye ni mwimbaji maarufu wa nyimbo za taarabu. Halima vilevile, anakataa kunaswa na mtego wa *Mwenye Meno* wa kumnunua kwa pesa. Anachukizwa na kitendo cha kulipiwa bili kwenye hoteli na mwanamume. Anafoka kwa hasira kwamba yeye na rafiki yake Shahida hawakwenda pale hotelini kuombaomba au kudoea pesa za mwanamume. Anakiona kitendo kile kama njia ya kumvunja mwanamke heshima. Aidha, anakataa kulitumia gari la kifahari aina ya *Mercedes Benz* alilonunuliwa na *Mwenye Meno*. *Mwenye Meno* alimwona kama mwanamke mgumu hivyo akaamua kumshawishi kwa kumnunulia gari la kifahari lakini Halima anashikilia msimamo wa kujiheshimu kama mwanamke. Nukuu ifuatayo inathibitisha hili:

Ndani ya miaka miwili, gari jipya la fahari alilotunukiwa Halima, limeganda palepale uwanjani lilipotupwa. Hata yale mapambo ya maua yaliyofungwa mbele ya gari yameoza na kukauka. ...Katika mapuuzi ya muda mrefu kama hivyo, mchezo wa vuta n'kuvute wa mtunuki na mtunukiwa, umeendelea kwa muda mrefu pia. Mtunuki hakuwa na subira hata kidogo, kwa hivyo, aliongeza kiburi tu, kumtuturisha moyo mtunukiwa akubali matakwa yake. Lakini wapi! Halima haukumpiga mshipa. (Said Ahmed, 83).

Hatimaye, Halima sawa na Nana, anafunga ndoa na Muuza Madafu ambaye amezaliwa na kukulia katika familia maskini.

Nana na Halima wanauasi mfumo wa ubabedume unaomtukuza mwanamume huku ukimdunisha mwanamke. Nana anamkabili baba yake bila woga na kudai uhuru wa kujifunza kuwa peke yake. Anatilia shaka kauli ya baba yake kuwa alihitaji kulindwa kwa sababu alikuwa mtoto wa kike. Anashangaa iwapo mtoto wa kiume pia hawezi kuharibika. Anapinga mfumo wa kuumeni unaowatazama wanaume kama masimba na mafisi huku wanawake wakiangaliwa kama paa, nyumbu au pundamilia. Nana anakataa kabisa kukubaliana na baba yake, anagoma kula na kuenda shule mpaka anapatiwa uhuru wake. (Uk. 38-39).

Katika waraka aliouandika kuhusu Halima, *Mwenye Meno* anakiri kwamba Halima alikuwa mwanamke huru. Tazama:

Aliandika mengi. Aliandika kuhusu uzuri wa Halima. Akasifu ushujaa wake. Akautukuza usomi wake. Akaukubali usafi wa nje na ndani ya nafsi yake. Akauweka juu ukweli wake. Akaubeba uhuru wake-uhuru usio na pesa, bali uhuru wa kusema anachotaka bila kuogopa. Uhuru wa heshima ya uke wake. Upeo na wasifu wa heba yake. Nani atakayekubali uhalisia wa mwanamke mpya katika dunia hii? Yupo! Muulize Halima! (Said Ahmed, 207).

Nana katika *Nyuso za Mwanamke* na Halima katika *Wenye Meno*, wanashiriki katika juhudi za kuipigania jamii yenye usawa na haki. Tunamwona Nana akihoji jinsi baba yake anavyojilimbikizia

utajiri wa haramu. Anawasitikia wakulima ambao hawajui wa kulalamikia baada ya kunyang'anywa ardhi na uhuru wao. Nana vilevie anatalia shaka utaratibu wa jinsi baba yake anavyopandishwa vyeo kazini. Anaeleza kuhusu utajiri wa baba yake ambao anasema kuwa baadhi ni halali na mwingine ni haramu. (Uk. 29).

Halima katika *Wenye Meno* anashangazwa na utajiri mkubwa wa Mwenye Meno. Haelewi anakotoa pesa zinazonyesha kama mvua ilhali kuna watu wengi ambao hawawezi kupata hata mlo mmoja kwa siku. Anakashifu vyombo vya dola ambavyo vinaficha majina ya watu wakubwa ambao wanaharibu maisha ya vijana kwa dawa za kulevywa. Halima anakataa kubaki kimya na kushiriki katika utafiti wa kufichua maovu haya. Anawahamasisha wanawake wenzake kuhusu mpango wa kumtia Mwenye Meno adabu. (Uk. 149).

Nana na Halima wanashiriki katika harakati za kuikomboa jamii kupitia vyombo vya habari. Nana anamiliki nyumba yenye ghorofa kumi inayojulikana kama *Karibu Mwanamke*. Katika ghorofa ya tano ya nyumba hii, kuna ofisi ya kitengo cha *Hifadhi ya Watoto na Vijana*. Hapa ndipo matatizo mbalimbali ya watoto yanapotatuliwa. Ghorofa ya sita ina kitengo cha *Matatizo ya Wanawake*. Mwanamke yeyote ambaye ana matatizo ya unyumba, kubaguliwa, kubakwa, kukandamizwa na mengineyo alisaidiwa hapa. Tunaambiwa kwamba hiki ndicho kilikuwa kitengo muhimu zaidi katika nyumba hii.

Kituo cha redio ya FM iliyoitwa *Uwazi* kilikuwa katika ghorofa ya saba. Majadiliano kuhusu kero za wananchi, majadiliano baina ya watangazaji na wasikilizaji na wasikilizaji na wasikilizaji yalifanyika katika redio hii. Kituo cha televisheni kilichojulikana kama *Televisheni Yetu* kilikuwa katika ghorofa ya nane. Mambo muhimu ya watu wa kawaida yalishughulikiwa katika runinga hii. Ofisi ya Nana ambaye alikuwa mkurugenzi ilikuwa katika ghorofa ya tatu. (Kur. 197-198).

Halima vilevile, anaendeleza harakati za kiukombozi kwa kushiriki katika utafiti wa kuwachunguza matajiri waliogeuka funza wa kuwadhulumu watoto kimapenzi. Utafiti ambao unaelezwa kuwa wenye ujasiri na hatari. Anachapisha matokeo ya utafiti wake kwenye gazeti la *Habari Motomoto*. (Uk. 20). Baada ya kufanya utafiti wa kina kuhusu maovu yaliyotekelezwa na Mwenye Meno, Halima anakusudia kuchapisha matokeo ya utafiti wake katika gazeti mashuhuri linalojulikana kama *Ukweli Mchungu*. (Uk.148). Kutokana na habari hizi, watu wanaanza kutazama jamii yao upya. Wanapata mwamko mpya wa kusimama kidete na kupigania haki zao. Kupitia wahusika hawa wawili (Nana na Halima), mwandishi anaonekana kumpa mwanamke kipaumbele katika harakati za kuipigania jamii yake.

Mwingilianomatini wa Uhusika

Mwandishi wa matini fulani anapotaka kumsawiri mhusika mwenye wasifu fulani katika matini yake, kuna uwezekano akilini mwake, awe na mhusika mwenye wasifu huohuo anayepatikana katika matini nyingine ya awali. (Allen 2000:12). Kwa mujibu wa kauli hii, mhusika wa matini ya sasa atakuwa na wasifu unaoshabihiana kwa kiwango fulani na yule wa matini tangulizi. Kuna mwingilianomatini katika usawiri wa wahusika katika kazi zote mbili. Mwingilianomatini huu unajitokeza ifuatavyo:

Mwingilianomatini wa Uhusika kati ya Nana na Halima

Mhusika Halima amesawiriwa kama mhusika Nana wa *Nyuso za Mwanamke*. Wahusika wote ni jasiri. Ujasiri wa Nana unajitokeza kwa namna anavyomjibu baba yake bila woga. Baba anataka kueleza aliyemwalika mpiga-gita kwenye sherehe. Nana anajibu kuwa ile ilikuwa sherehe yake na alikuwa na haki ya kumwalika mtu yeyote. Katika sherehe hiyohiyo, iliyokuwa na watu wenye vyeo kama baba yake, Nana anapiga gilasi kuwanyamazisha watu ili mpiga-gita aimbe wimbo. (Kur. 53-54).

Ujasiri wa Nana unadhihirika anapokaidi taratibu zinazohusishwa na miadi ya kuwaona viongozi. Sekretari anapomkataza kuonana na meneja wa hoteli ya *Crescent* bila miadi, Nana anamtuma kwa huyo boshi wake amjuzue kuwa miadi huvunjwa na dharura. Hatimaye anafululiza hadi ofisini. Mazungumzo baina ya Nana na meneja yanamsawiri kama mwanamke jasiri asiyeweza kutishwa na hadhi, uwanaume au pesa. Anapinga majina yanayotumiwa na meneja kumkunisha mwanamke kama vile 'Kimwana'. Ujasiri huu unajitokeza ifuatavyo:

“Kamwambie boshi wako, miadi huvunjwa na dharura.”

Alitamka kwa hamaki Nana. Sekretari akarudisha karipio kwa Nana, “Mimi nimeshakwambia huwezi kumwona ovyoovyo, basi nd’o huwezi kumwona. Huwezi kumwona hata kwa mizinga...”

“Bibi we, mzinga ni mimi mwenyewe! Naweza kuripuka na kupasuka.” Nana alijibu huku akifululiza ndani kwa boshi.

“...nitakuitia polisi. Wacha ukavu.”

“Niitie hata jeshi lote la wananchi, kwani ukavu ndio mtindo wa siku hizi.” (Said Ahmed, 161-162)

Nana anamtia adabu mhusika anayejulikana kama Ngware kwa kumpiga kiasi cha kulazwa hospitalini. Anathibitisha kwamba mwanamke ana uwezo wa kujikinga dhidi ya dhuluma kutoka kwa mwanamume. Baada ya kumpiga, Nana anamlipia gharama ya hospitali. (Uk. 274).

Halima katika riwaya ya *Wenye Meno* anakiri kwamba yeye ni mtu jasiri. Anasema kwamba uke wake hauwezi kumfanya aogope wala kuchelea kusema analotaka. Ujasiri wa Halima unadhihirika katika nukuu hii:

“Kupita nilipita kweli Shahida, lakini kwa nguvu na ukakamavu wangu. Ukakamavu Shahida ni moja kati ya ‘anuwai’ za nguvu. Panapo kiburi na wewe tia kiburi. Lazima ukusanye nguvu. Uwongo na njama nimezikwepa kwa nguvu na kukataa. Mimi siogopi wala sichelei kusema kwa uke wangu. (Said Ahmed, 14).

Halima vilevile, haogopi kukabiliana na watu wenye mamlaka na pesa. Anashiriki katika mada inayoelezwa kama ya ujasiri na hatari. Hata hivyo, tunaambiwa kuwa, ujasiri na hatari ilikuwa kazi ya Halima kama tunavyoelezwa hapa:

Selesele alitaka kusema yasiyotakiwa kusemwa. Yaani sakata ya funza wanaomega uke na uume wa vitoto vidogo vya shule, mitaani na vyuoni. Mada ambayo Halima aliitafiti na kuiandika kwenye gazeti la *Habari Motomoto*. Ilijulikana na kila mwananchi. Ilikuwa mada ya ujasiri na hatari, lakini ujasiri na hatari ilikuwa kazi yake. Kwa hivyo hakuogopa kujitia motoni ili atoke furahani. (Said Ahmed, 20).

Katika kuelezea sifa za Halima, Mwenye Meno anamwona kama jasiri asiyeogopa, shujaa na msomi. (Uk. 207).

Wahusika Nana na Halima wametumika kimwingilianomatini kama wanamapinduzi. Wawili hawa ni wanaharakati ambao wanapigania ujenzi wa jamii mpya yenye haki na usawa. Aidha, wanaendeleza juhudi za kumkomboa mwanamke katika jamii zao. Nana amesawiriwa kama mtetezi wa wanyonge. Tunamwona akihoji jinsi baba yake- Bwana Hila, anavyojilimbikizia utajiri wa haramu. Anawasitikia wakulima ambao hawajui wa kumlalamikia baada ya kunyang’anywa ardhi na uhuru wao. (Uk. 37). Halima katika riwaya ya *Wenye Meno* anahoji kiini cha utajiri wa Mwenye Meno. Anashangazwa na jinsi anavyotumia pesa nyingi kwenye anasa ilhali wapo maskini wengi wanaokosa hata mlo mmoja kwa siku. (Uk. 84).

Nana anakumbuka mhadhara alioutoa juu ya mageuzi katika maendeleo ya jamii. Mhadhara ambao ulimzidishia uadui miongoni mwa waratibu na wasomi wanaolipwa pesa nyingi na mashirika yasiyokuwa ya serikali. Tunaeleza:

Mara Nana alikumbuka mhadhara alioutoa hivi juzi, yaani *juzi ya kijomba*; mhadhara juu ya mageuzi katika maendeleo ya jamii, ambao, kwa upande mmoja, ulizidi kumpa umaarufu kwa wanawake walengwa, lakini kwa upande wa pili, ulimzidishia uadui miongoni mwa waratibu na wasomi wanaolipwa chungu ya pesa na *non-governmental organisations*. (Said Ahmed, 191).

Nyumba anayomiliki Nana ya *Karibu Mwanamke*, imetengewa vitengo tofautitofauti vya kuendeleza shughuli za haki na usawa katika jamii. Mathalani, kuna vitengo vya kuangazia matatizo ya watoto, wanawake, maskini na kero zinazowakumba wananchi. Masuala haya yote yanashughulikiwa chini ya uongozi wa Nana ambaye ndiye mkurugenzi. Tunaelezwa:

Kwa wakati huu Nana tunamkuta ofisini mwake akijitayarisha kwenda kwenye mjadala wa matatizo ya wanawake. (Said Ahmed, 198).

Halima pia amesawiriwa kama Nana; mwanaharakati anayejihusisha na utafiti wa kuyafichua maovu katika jamii. Mwanzoni mwa riwaya, Halima anatoa kauli ya kuwahamasisha wanyonge walio wengi kuungana. Anasema kwamba hata maskini na mafukara wana nguvu zao kama tunavyoeleza katika kifungu hiki:

“Hata maskini na mafukara wana nguvu zao pia. Nguvu yao kubwa ni umoja. Nguvu za wingi wa raia. Nguvu za kukataa mateso na udhalilishaji. Nguvu za kususia. Nguvu za kutoogopa. Nguvu za uzalendo. Nguvu za sisi dhidi yao. Nguvu za hohehahe na mabwana wakubwa. Nguvu za akina sisi wanawake na wanaume. Nguvu zipo shoga yangu. Zipo nguvu! Nguvu zipo utake usitake!” (Said Ahmed, 9).

Halima anafanya juhudi za kutafuta habari kuhusu Mwenye Meno. Hii ni baada ya kutilia shaka utajiri wake na jinsi anavyoandamana na walinzi wengi. Anafanya mahojiano na watu wengi akiwamo kijana mmoja kwa jina Kama Sudi. Kama Sudi ni kijana anayefanya biashara ya kununua magari kutoka nje na kuyauza nchini. Kijana huyu alikuwa na uhusiano wa karibu na waheshimiwa vigogo. Tunaelezwa kuwa mazungumzo baina ya Halima na Kama Sudi yalihusu mambo yaliyowakereketa wananchi hasa wale waliokuwa maskini hohehahe. Tunaambiwa:

Walizungumza mambo mengi muhimu ya waziwazi yanayowakereketa wananchi, hasa wale walio hohehahe. Walizungumza kuhusu sheria na jinsi zinavyopindwa au kukanyagwa na kisha kutupwa. Pia walizungumza kuhusu jinsi heshima ilivyopotea baina ya watawala na watawaliwa. Si hayo tu, walijadiliana kuhusu ukosefu wa ajira, kudorora kwa viwango vya elimu na kulegea kwa mfumo wa afya na matibabu. (Said Ahmed, 50-51).

Mwingilianomatini wa Uhusika kati ya Bwana Hila na Mwenye Meno

Wahusika hawa ni wahusika wakuu katika riwaya tunazohakiki. Misukumo na matendo ya Bw. Hila na Mwenye Meno yanadhihirisha kuwa wahusika hawa wanaingiliana kisifa. Wao ni watu fisadi. Tamaa yao ya mali ya umma haina kikomo. Bwana Hila ni kiongozi anayejilimbikizia utajiri mwingi kwa njia haramu. Nana ana haya ya kusema kuhusu baba yake:

...Mafukara ndiyo, lakini si wajinga! Hawana la kufanya ndio, bali wanawachukia watu kama babangu kwa utajiri wa haramu wanaozidi kujilimbikizia. Na si utajiri tu, bali nguvu, na si nguvu tu, bali jeuri na ukatili unaotokana na ulimbukeni wao. (Said Ahmed, 36-37).

Kulingana na Nana, baba yake ni miongoni mwa viongozi fisadi. Anasema kuwa watu wakubwa akiwemo baba yake, walikuwa na mitaji mingi ambayo uhalali wake ulitiliwa shaka. Baadhi ilikuwa mitaji ya siri ijapokuwa ilihalalishwa kichinichini na serikali. (Uk. 29). Nana vilevile, analalamikia tabia ya baba yake ya kutumia pesa katika anasa ilhali watu wengi wamezama katika ufukara. Bwana Hila anatumia pesa nyingi katika sherehe za kila aina ambazo kulingana na bintiye, hazina maana yoyote.

Mwenye Meno katika riwaya ya *Wenye Meno* ni kiongozi fisadi kama Bwana Hila. Ana utajiri mkubwa ambao haujulikani chanzo chake. Isitoshe, anatumia utajiri huu kujistarehesha wakati watu wengi katika jamii yake wanaangamia kwa njaa. (Uk. 84). Mwenye Meno anaungama kuwa mfumo

unaotawala dunia ni mfumo unaoshabikia ufisadi. Mfumo unaozalisha mabwenyenye wachache wanaowadhulumu maskini walio wengi. Anasema:

“Tunaambiwa kuwa mfumo unaotawala wa dunia hii ni demokrasia, wenye maana ya mfumo wa watu, kwa ajili ya watu na kwa maslahi ya watu. Tazama sasa mparaganyiko wa mambo unavyokwenda sambamba na nguvu za watu wachache wanaosukuma umati wa watu ili wafanikiwe wao na watoto wao na wale walio karibu na wao wanaowatupia makapi.” Said Ahmed, 206-207).

Wanaume hawa ni wahusika wa kimwingilianomatini, ni wenye kiburi, mabezo na matusi. Bwana Hila anawarejelea watu wa tabaka la chini kama watu duni wasio na kipato kabisa. Anamsuta binti yake kwa kumthamini Mpiga-gita asiyekuwa na chochote. Anamlinganisha na takataka zinazotupwa jaani. Mwenye Meno naye anaangua kicheko anapotazama na kusikiliza malalamishi ya wananchi. Anasema kuwa usasa wa dunia unampa raha yule mwenye pesa. Anawasuta wananchi kwa kutoa vilio ambavyo kamwe haviwezi kuwafikia matajiri pindi wanapoingia kwenye magari na kufunga vioo. Nukuu zifuatazo zinathibitisha haya:

“Vitendo vyako siku hizi vinaashiria uovu. Vinavimba polepole na kutaka kutibua wimbi. Mama yako alitoka kwangu Kwenda kuthamini watu duni wasio kipato kabisa, wanaogaragara na vumbi. Na wewe unamthamini huyu mpiga-gita badala ya mtoto wa mfanyabiashara mashuhuri-unamwambaa Dusa! Kwa nini unathamini takataka, tena takataka zinazotupwa jaani?” (Said Ahmed, 47).

Mwenye Meno alitengeneza kicheko chake mwenyewe. Akakirambisha tamu ya asali. Unajua? Usasa wa dunia yetu unampa raha mwenye pesa. Tazama wale wanaoitwa wananchi badala ya wasiokuwa-wananchi. Tazama jinsi wanavyoropokwa na kucharukwa. Hakuna Mwenye Meno hata mmoja anayesikia maneno yao, kwani maneno hayo hayaingii ndani ya gari wakishafunga vioo. (Said Ahmed, 191).

Mwingilianomatini wa uhusika unabainika kwa namna ambavyo Bw. Hila na Mwenye Meno wanavyohusiana na jinsia ya kike. Kwao, mwanamke ni chombo cha kumstarehesha mwanamume. Wanatumia pesa nyingi kuwashawishi wanawake kimapenzi. Kulingana na Bi. Mkubwa (mamaye Nana), Bwana Hila alidhani kuwa maisha ya mwanamke ni kustareheshwa. Tazama:

...bwana huyo alidhani kwamba maisha ya mwanamke ni kustareheshwa. Mwanamke ni pambo tu la nyumba kwa hivyo anachostahiki ni kupewa kila kitu anachokitaka isipokuwa kutoka nje ya nyumba. Apewe mavazi ya fahari, manukato ghali, chakula cha rutuba, watumishi wa kila kitu mpaka wa kumfulia chupi zake. Gari la kusafiria na bwana, pesa za masurufu au kununulia anachopenda...mradi tu mwanamke abaki ndani kungoja kumstarehesha bwana. Lazima afugwe ndani. (Said Ahmed, 287).

Tunaambiwa kuwa mchezo mkubwa wa Mwenye Meno ulikuwa kuagiza vipusa vya wanawake. Anatomia pesa nyingi kununua miili ya wanawake mintarafu ya kujipa starehe. Anamwomba mpenzi wake-Shahida, ruhusa ya kuvunja ahadi ya penzi lao ili apate kujistarehesha na wanawake wenzake. (Uk. 138).

Hitimisho

Makala hii imeshughulikia mwingilianomatini katika riwaya mbili za Said Ahmed Mohamed tulizoteua maksudi. Tumeonyesha kwamba riwaya hizi zinaingiliana na kurejeleana katika vipengele vya maudhui na uhusika. Aidha, imebainika kuwa, kuakisika kwa nduni sawia za kiutunzi baina ya riwaya ya *Nyuso za Mwanamke* na *Wenye Meno*, ni ufundi anaotumia mwandishi kukuza na

kuimarisha mbinu zake za kiutunzi. Hii ni kwa sababu kazi za kifasihi hukumbushana, huingiliana na husaidiana na kwa namna nyingine huweka upya fulani katika kitu kilekile cha zamani. Aidha, Said Ahmed anapokariri baadhi ya nduni za kiutunzi za riwaya ya *Nyuso za Mwanamke* katika riwaya ya *Wenye Meno* (kwa kukusudia au kutokusudia), anachangia katika uchambuzi na uelewekaji wa riwaya ya *Wenye Meno*. Hivyo, maana ya matini ya kifasihi haiwezi kuangaliwa kivyake bila kuhusishwa na matini nyingine ya awali kama inavyosema Nadharia ya Mwingilianomatini.

Marejeleo

- Allen, G. (2000). *Intertextuality*. New York: Routledge.
- Bakhtin, M. (1981). *The Dialogic Imagination: Four Essays*. Austin & London: University of Texas.
- Chimerah, R na Njogu, K. (1999). *Ufundishaji wa Fasibi: Nadharia na Mbinu*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
- Eagleton, M. (1991). *Feminist Literary Criticism*. London: Longman.
- Grass, Gunter. (1962). *The Tin Drum*. Tafsiri ya Ralph Manheim. New York: Vintage.
- Kristeva, J. (1980). *Desire in Language: A Semiotic approach to Literature and Art*. New York: Colombia University Press.
- Mohamed, S. A. (1977). *Asali Chungu*. Nairobi: Shungwaya Publishers.
- Mohamed, S. A. (1980). *Utengano*. Nairobi: Longman.
- Mohamed, S. A. (1980). *Dunia Mti Mkavu*. Nairobi: Longhorn Publishers.
- Mohamed, S. A. (1988). *Kiza Katika Nuru*. Nairobi: Oxford University Press.
- Mohamed, S. A. (1990). *Tata za Asumini*. Nairobi: Longhorn Publishers.
- Mohamed, S. A. (2001). *Babu Alipofufuka*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
- Mohamed, S. A. (2006). *Dunia Yao*. Nairobi: Oxford University Press.
- Mohamed, S. A. (2010). *Nyuso Za Mwanamke*. Nairobi: Longhorn Publishers.
- Mohamed, S. A. (2012). *Mbanga Nafsi Yangu*. Nairobi: Longhorn Publishers.
- Mohamed, S. A. (2013). *Mkamandume*. Nairobi: Longhorn Publishers.
- Mohamed, S. A. (2014). *Kamwe si mbali tena*. Nairobi: Oxford University Press.
- Mohamed, S. A. (2018). *Wenye Meno*. Nairobi: Spotlight Publishers.
- Naveen, K.J. na Akshatha, D. S. (2021), 'The Role of Women in Today's Society,' Volume 9-6 pp: 32-37, ISSN (online). Available at www.questjournals.org.
- Njogu, K na Wafula, R.M (2007). *Nadharia za Ubakiki wa Fasibi*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
- Wamitila, K. W. (2008). *Kanzi ya Fasibi. Misingi ya Uchanganuzi wa Fasibi*. Nairobi: Vide-Muwa Publishers Ltd.